

Tamko na Sala ya kuukana udanganyifu

Ninakushukuru Baba kwa kuwa wewe ni Mungu wa ukweli, na kuwa wewe unaiangazia nuru yako katikati ya usiku wenye giza nene, ili nikae katika nuru yako.

Nakusihi tafadhali unisamehe kwa uongo wote niliousema. Mara nyingi nimechagua njia ya kupata faraja na kile kilicho rahisi, na si kilicho sahihi na haki. Nakuomba ee Bwana uisafishe midomo yangu iondokane na kutomcha Mungu katika mambo yote. Unipe moyo unaofurahia kusikia ukweli, na kinywa kilicho tayari kuufanya ukweli ujulikane kwa wengine.

Unipe ujasiri kufarijika katika ukweli, na kuukataa uongo.

Leo hii nakataa na kuyakana matumizi ya uongo katika maisha yangu ya kila siku.

Nayakataa mafundisho yote ya Kiislamu ambayo yanatumika kuhalalisha kusema uongo, ikiwa ni pamoja na taqiyya. Naamua kuachana na uongo wote na udanganyifu. Nachagua kuishi katika ukweli.

Natangaza kuwa Yesu Kristo ndiye Njia, Kweli na Uzima. Nachagua kuishi chini ya ulinzi wa kweli yake.

Ninatangaza kuwa usalama wangu uko ndani yako, na kuwa Kweli itaniweka huru.

Tafadhali nakusihi Baba wa mbinguni nionyeshe namna ya kuenenda katika nuru ya kweli yako. Unipe maneno ya kusema; na njia nitakayoiondea, ambayo msingi wake ni kweli yako.

Amina.